Hakika Misikiti hii haifai kuwekwa chochote katika mikojo hii, wala uchafu wowote, bali hii ni kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuswali, na kusoma Qur'ani

Imepokelewa kutoka kwa Anas bin Maalik -radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Siku moja sisi tukiwa Msikitini pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake ghafla akaja bedui, akasimama akaanza kukojoa Msikitini, wakasema Maswahaba wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Koma, koma!, anasema: Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Msimkatishe, muacheni" Wakamuacha mpaka akamaliza kukojoa, kisha baada ya hapo Mtume rehema na amani ziwe juu yake akamuita, akasema kumuambia: "Hakika Misikiti hii haifai kuwekwa chochote katika mikojo hii, wala uchafu wowote, bali hii ni kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kuswali, na kusoma Qur'ani" Au kama alivyosema Mtume rehema na amani ziwe juu yake, anasema; akumuamrisha mtu mmoja miongoni mwao akaja na ndoo ya maji akapamwagia.

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake msikitini kwake akiwa pamoja na Maswahaba zake, akaja bedui mmoja kutoka kijijini, akaanza kukojoa katika kona ya msikiti. Maswahaba wakamkaripia na wakasema: Koma, na wacha unachokifanya. Akasema rehema na amani ziwe juu yake: Muacheni, na wala msimkatishe mkojo wake, wakamuacha mpaka akamaliza. Kisha rehema na amani ziwe juu yake akamuita na akamwambia: Hakika misikiti haifai kwa chochote miongoni mwa mikojo hii, wala aina yoyote ya uchafu, bali ni kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na kutukuka, na swala, na kusoma Qur'ani na mfano wa hayo. Kisha akamuamrisha rehema na amani ziwe juu yake mtu mmoja katika Maswahaba akaja na ndoo iliyojaa maji akayamwaga katika mkojo wake.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/8948